**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**OFISI YA MAKAMU WA RAIS**

# HOTUBA YA MHE. DKT. PHILIP ISDOR MPANGO, MAKAMU WA RAIS WA JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA, KWENYE KILELE CHA MAADHIMISHO YA SIKU YA MAZINGIRA DUNIANI, 2025

**UKUMBI WA MIKUTANO WA JAKAYA KIKWETE, DODOMA**
**5 JUNI, 2025**

**Jamhuri ya Muungano wa Tanzania!**

Napenda kuanza kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu aliyetujalia uzima na afya njema, na kutuweza kukusanyika hapa kuadhimisha siku ya mazingira duniani. Naipongeza Ofisi ya Makamu wa Rais, uongozi wa Mkoa wa Dodoma, mikoa ya jirani, na wadau mbalimbali kwa maandalizi mazuri ya maadhimisho haya. Vilevile, nawashukuru nyote kwa kutenga muda wenu na kushiriki katika maadhimisho haya. Ukubwa wa hadhira hii unaashiria uelewa na matamanio tuliyonayo ya kuendeleza jukumu la msingi la kuhifadhi mazingira na kudumisha maendeleo endelevu nchini.

***Wahe. Viongozi na Ndugu Wananchi;***

Suala la usimamizi na uhifadhi wa mazingira ni kipaumbele katika maendeleo ya nchi yetu. Hata hivyo, Taarifa ya Nne ya Mazingira ya Mwaka 2024 inaonesha kuwa hali ya utunzaji na uhifadhi wa mazingira nchini bado hairidhishi. Nchi yetu inaendelea kukabiliwa na changamoto mbalimbali za uharibifu wa mazingira ambazo kwa kiasi kikubwa zinatokana na tabiawatu. Uchafuzi wa mazingira umekuwa tishio na kichocheo cha ongezeko la majanga mengine mawili ya kimazingira duniani, ambayo ni mabadiliko ya tabianchi na upotevu wa bayoanuai. Shirika la Umoja wa Mataifa la masuala ya mazingira (UNEP) linakadiria kuwa takriban tani million 11 za taka za plastiki duniani hutelekezwa na kuhatarisha mifumo ya ikolojia, ikiwemo kuongezeka kwa joto na kudhuru afya ya udongo, bahari, Maziwa na mito. Hasara inayotokana na uharibifu huu kijamii na kimazingira duniani, inakadiriwa kuwa kati ya dola za Marekani bilioni 300-600 kwa mwaka. Vilevile, tishio hili kwa nchi zinazoendelea ikiwemo Tanzania, linaongezeka kwa kasi kubwa, siyo tu kutokana na taka tunazozalisha wenyewe, bali na nyingine nyingi zinazotupwa baharini.

Maadhimisho haya ambayo ni sehemu ya jitihada za Jumuiya ya Kimataifa kutambua umuhimu wa kuhifadhi mazingira na kutukumbusha wajibu wetu katika suala hilo, yanaongozwa na Kaulimbiu ya kimataifa isemayo ***"Komesha Uchafuzi wa Mazingira Unaochangiwa na Taka za Plastiki".*** Na kitaifa, maadhimisho haya yanabeba kaulimbiu isemayo ***"Mazingira Yetu na Tanzania Ijayo, Tuwajibike Sasa: Dhibiti Matumizi ya Plastiki".*** Kaulimbiu hizi zimechaguliwa ili kuchagiza jitihada za kuhamasisha jamii ya kimataifa na wananchi kwa ujumla kulinda vyanzo vya maji na mazingira, dhidi ya athari za taka za plastiki na kupunguza matumizi ya bidhaa za plastiki kupitia uzalishaji na ulaji endelevu.

***Wahe. Viongozi na Ndugu Wananchi;***

Miji na Majiji yetu bado yanakabiliwa na changamoto ya kushindwa kudhibiti taka ngumu na hivyo kupelekea uharibifu wa mazingira na vyanzo vya maji. Takwimu zilizopo zinaonesha kuwa, hivi sasa nchi yetu inazalisha takriban tani million 17.4 za taka ngumu kila mwaka, na 50% tu kati ya hizo, ndiyo inayokusanywa na kudhibitiwa kwa njia mbalimbali ikiwemo urejelezaji kwa matumizi mengine. Inakadiriwa kuwa ifikapo mwishoni mwa mwaka 2025, uzalishaji wa taka ngumu utafikia tani million 21.7. Aidha, kiasi cha taka kisichokusanywa na kutupwa au kurejelezwa ipasavyo huchangia takribani 40% ya mzigo wa magonjwa kwa Taifa. Pia, urejelezaji wa taka bado ni wa kiwango cha chini kutokana na sababu mbalimbali ikiwemo hamasa ndogo ya wadau katika kuchangamkia fursa mbalimbali zitokanazo na uchakataji taka. Kwa ujumla, menejimenti ya taka ngumu hapa nchini inakabiliwa na changamoto mbalimbali, zikiwemo ongezeko kubwa la kiasi cha

taka kinachozalishwa, miundombinu hafifu ya uzoaji taka, na teknolojia duni. Mathalan, utafiti uliofanywa na DfID mwaka 2019 katika jiji la Dar es salaam ulionesha kuwa takriban tani 508.8 za taka za plastiki hazikusanywi wala kurejelezwa. Hali hii husababisha hasara kiuchumi inayokadiriwa kufikia Dola za Marekani 27,856,800.

Hatua kadhaa zimechukuliwa ili kukabiliana na changamoto ya taka ngumu za plastiki na kuimarisha udhibiti wa taka kwa ujumla. Baadhi ya hatua hizo ni pamoja na kuweka katazo la matumizi ya mifuko na vifungashio vya plastiki ambalo limewezesha kuondolewa kwa zaidi ya mifuko ya plastiki 750,000 Tanzania Bara na Zanzibar, kushirikisha wadau mbalimbali, ambapo takriban makampuni 8 yameweza kuungana kuunda umoja ujulikanao kama PETCO (Polyethylene Terephthalate Recycle Company). Kupitia umoja huo, zaidi ya tani million 12.5 za taka za plastiki zimekusanywa na kurejelezwa; Vilevile, umoja huo umewezesha kupatikana kwa ajira zaidi ya 5,000, zinazojumuisha wakusanya taka mitaani. Aidha, mikakati kadhaa imebuniwa ili kuhamasisha matumizi ya fursa zitokanazo na uchakataji wa taka za plastiki na kuhamasisha Uchumi unaozingatia uzalishaji kidogo wa taka za plastiki. Baadhi ya mikakati hiyo ni pamoja na Wajibu wa Wazalishaji (Extended Producer Responsibility – EPR); Mwongozo wa menejimenti ya taka (2019), na mkakati wa R3 (Reuse, Reduce and Recycle).

***Wahe. Viongozi na Ndugu Wananchi;***
Ripoti ya mwaka 2023 ya Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Mazingira (UNEP), ilibainisha kuwa uchafuzi wa plastiki unaweza kupunguzwa hadi 80% ifikapo mwaka wa 2040 endapo nchi na wadau wa mazingira zitaweka sera thabiti na kufanya mabadiliko katika uuzaji wa bidhaa katika masoko kwa kutumia teknojia iliyopo. Kwa mujibu wa Ripoti hiyo, mabadiliko yanayohitajika ili kukomesha uchafuzi wa plastiki ni pamoja na kukuza uchumi unaotumia bidhaa tena na tena (re-use) ili kuzuia plastiki kwenye mifumo ya ikolojia na katika uchumi. Kimsingi utumiaji tena na tena, unaojumuisha chupa zinazoweza kujazwa upya, dispensa kubwa, mipango ya kurejesha mifuko n.k. unaweza kupunguza 30% ya uchafuzi wa plastiki ifikapo mwaka 2040. Hali kadhalika, inawezekana kupunguza uchafuzi wa plastiki iwapo urejelezaji utaimarishwa kwa kutekeleza yaliyomo kwenye mwongozo wa kukuza uchakataji, na hivyo kuongeza kiwango cha plastiki inayoweza kuchakatwa kutoka 21% hadi 50%. Aidha, matumizi mapya na matumizi ya mifuko ya plastiki na bidhaa zilizotengenezwa kutokana na nyenzo mbadala (kama vile karatasi au vitu vinavyoweza kuoza, plastiki iliyochakatwa, n.k.) yanaweza kupunguza 17% ya ziada ya uchafuzi wa plastiki.

***Wahe. Viongozi na Ndugu Wananchi;***
Nichukue fursa hii kutoa wito kwa wadau wote wa mazingira kuendeleza mambo yote yaliyofanyika katika maadhimisho haya, ikiwa ni pamoja na upandaji miti na uanzishwaji wa bustani za kijani, kuhamasisha matumizi ya teknolojia za urejelezaji wa taka ozo na za plastiki, kupunguza ukataji miti holela kwa ajili ya kuni na mkaa, na kuongeza matumizi ya nishati safi ya kupikia. Matumizi makubwa ya kuni na mkaa yanachangia athari za mazingira, kiafya, kijamii na kiuchumi. Kutokana na hali hiyo Serikali imeweka nia ya kupunguza athari hizo kwa kupunguza matumizi ya nishati ya kuni na mkaa kwa shughuli za kupikia. Katika kutekeleza nia hiyo, Serikali ilitoa katazo la matumizi ya kuni na mkaa kwa taasisi zinazoandaa chakula na kulisha watu zaidi ya watu mia moja kwa siku, kuanzia tarehe 31 Januari, 2024, na kuzitaka zihamie katika matumizi ya nishati safi ya kupikia.

Taarifa zilizopo zinaonesha kuwa Taasisi nyingi za Serikali na binafsi zimeanza kutekeleza katazo hilo na kuanza kutumia nishati safi ya kupikia. Hadi kufikia Machi 2025 jumla ya taasisi 762 zilikuwa zimeanza kutumia nishati safi ya kupikia, kati ya hizo taasisi za umma ni 495 na taasisi binafsi ni 267. Taasisi za Serikali ni pamoja na zilizo chini ya OR-TAMISEMI (Taasisi 508); Wizara ya Mambo ya Ndani (Taasisi 58); Wizara ya Afya (Taasisi 26); Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia (Taasisi 123); Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum (Taasisi 13); na, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa (Taasisi 34). Nazipongeza Taasisi zote zilizotekeleza katazo hili na natoa rai kwa Taasisi ambazo bado hazijatekeleza, kuendelea kuwekeza katika matumizi ya nishati safi ya kupikia. Aidha, taasisi binafsi zinazolisha zaidi ya watu 100 nazo ziongeze kasi katika kutumia nishati safi ya kupikia ili kuokoa mazingira yetu na kulinda afya ya jamii.

***Wahe. Viongozi na Ndugu Wananchi;***

Nchi yetu imebarikiwa kuwa na utajiri mkubwa wa maliasili ambapo takriban hekta milioni 48.1 ni misitu ambayo ni sawa na wastani wa 55% ya eneo lote la nchi kavu. Misitu hii ni makazi ya viumbe hai na baadhi yake ni vyanzo vya maji ambayo ni muhimu katika ustawi wa maisha yetu na maendeleo yetu kiuchumi. Mbali na uzuri huu, taarifa mbalimbali za hali ya mazingira nchini zimedhihirisha kuwepo kwa uharibifu wa ardhi katika maeneo mbalimbali nchini, ambapo inakadiriwa kuwa takriban 61% ya ardhi nchini iko katika hatari ya kuharibika. Uharibifu huo pia umeongezeka zaidi kutokana na kuwepo kwa athari za mabadiliko ya tabianchi ambapo maeneo ya nchi yenye hali ya mvua chache yamezidi kukumbwa na ukame na hivyo kushuka kwa uzalishaji wa mazao ya kilimo na kutishia usalama wa chakula katika maeneo hayo. Uharibifu huu unachangiwa kwa kiasi kikubwa na shughuli za kibinadamu zisizo endelevu; idadi kubwa ya mifugo isiyolingana na uwezo wa malisho; ukataji wa misitu kwa ajili ya kuni na mkaa; uanzishaji wa mashamba mapya unaotokana na kilimo cha kuhamahama; na uchimbaji holela wa madini pamoja na upanuzi wa makazi usiozingatia mipango miji.

***Wahe. Viongozi na Ndugu Wananchi;***

Tafiti pia zimebainisha kuwa kila mwaka nchi yetu hupoteza wastani wa takriban hekta 469,420 za misitu. Upotevu huo wa misitu umepelekea upotevu mkubwa wa bayoanuai na hatari ya kutoweka kwa baadhi ya aina muhimu na adimu za jamii ya mimea na wanyama. Aidha, tathmini ya Wizara ya Maliasili na Utalii inaonesha kuwa hali ya uharibifu ikiendelea kama ilivyo, ifikapo mwaka 2033, uharibifu wa misitu utakuwa umeigharimu Serikali kiasi cha bilioni 167. Pia, inakadiriwa kuwa upotevu wa bioanuai ukiendelea, utaigharimu Serikali wastani wa 5% ya Pato la Taifa kwa mwaka na kuathiri zaidi jamii maskini za vijijini ambazo hutegemea mazingira na maliasili kwa maisha yao ya kila siku. Hali hii inatupa picha ya hali ya uoto wa asili na mazingira yetu kwa siku za usoni, ambapi inakadiriwa kuwa katika 50 ijayo, uharibifu huu wa ardhi usipodhibitiwa unaweza kuleta hatari ya kugeuka kuwa jangwa.

***Wahe. Viongozi na Ndugu Wananchi;***

Katika kukabiliana na uharibifu wa mazingira, Serikali imechukua hatua mbalimbali za kisera na kimkakati ikiwa ni pamoja na: kupitishwa kwa Sera ya Taifa ya Mazingira ya mwaka 2021; Mpango Kabambe wa Taifa wa Hifadhi na Usimamizi wa Mazingira (2022-2032); Sheria, Mikakati, miongozo inayohusu masuala ya mazingira; kuongezeka kwa kasi

ya upimaji wa ardhi na umilikishaji wa ardhi kimila; uhamasishaji wa matumizi endelevu ya ardhi hususan kilimo mseto, kilimo cha matuta, kilimo hifadhi na mbinu endelevu za kiasili za hifadhi ya malisho. Ili kuleta matokeo tarajiwa, naelekeza Wizara, Taasisi na Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini kuongeza kasi ya usimamizi na utekelezaji wa hatua hizi ikiwa ni pamoja na kuendelea kuhamasisha utunzaji wa mazingira kwa ujumla.

Jukumu la kuhamasisha na kuelimisha jamii kuhusu umuhimu wa hifadhi ya mazingira linahitaji ushirikiano wa wadau wote katika ngazi zote. Kipekee, natoa wito kwa vyombo vya habari, taasisi zote za Serikali & binafsi na asasi za kiraia kushirikiana katika kutoa elimu kwa jamii. Tukifanya hivyo, tutapunguza uharibifu wa mazingira hapa nchini kwa kiasi kikubwa.

***Wahe. Viongozi na Ndugu Wananchi;***

Kabla sijahitimisha hotuba yangu, napenda kuushukuru tena uongozi wa Mkoa na jiji la Dodoma kwa kukubali kwa mara nyingine tena kuwa mwenyeji wa maadhimisho ya siku ya mazingira duniani mwaka huu. Aidha, nawashukuru wananchi wote walioshiriki shughuli mbalimbali za maadhimisho haya pamoja na wadau wote waliochangia kwa namna moja ama nyingine katika kufanikisha maadhimisho haya. Kwa namna ya pekee natoa pongezi kwa vyombo vya habari ambavyo vimeendelea kuelimisha na kuhamasisha umma kushiriki katika shughuli za kuhifadhi mazingira. Ushirikiano huu muhimu unapaswa kuendelezwa kwa ajili ya kusukuma mbele mipango mbalimbali ya maendeleo ya Taifa letu, kwa kuwa vyombo vya habari ni muhimu katika kukuza uelewa na kuhamasisha jamii kushiriki katika shughuli za maendeleo.

Mwisho, naomba niwakumbushe kuhusu kushiriki kikamilifu kwenye Uchaguzi Mkuu wa Rais, Wabunge na Madiwani unaotarajiwa kufanyika mwaka huu. Ninawahimiza kushiriki uchaguzi huo kwa kugombea nafasi mbalimbali za uongozi, kushiriki kampeni ili kusikiliza sera za wagombea, na kujitokeza kupiga kura siku ya uchaguzi. Aidha, katika ushiriki huo nawasihi kudumisha hali ya utulivu na usalama hususan katika hatua ya uteuzi wa wagombea, kampeni za uchaguzi, upigaji kura na hata baada ya matokeo kutangazwa.

***Wahe. Viongozi na Ndugu Wananchi;***

Baada ya kusema hayo, ninayo heshima kwa niaba ya Mhe. Dkt. Samia Suluhu Hassan, Rais wa Jamhuri ya Muungano Tanzania, kutamka kuwa Maadhimisho ya Siku ya Mazingira Duniani mwaka 2025 yamefikia Kilele.

Asanteni sana kwa kunisikiliza.